

SAYANSI YA UVUMILIVU



KUONESHA UVUMILIVU HUWAFANYA WATOTO WAHISI KWAMBA WANATUNZWA NA KUPENDWA. HII NI MUHIMU KATIKA KUJENGA MAHUSIANO YENYE MAANA NA MAWASILIANO MAZURI.

TAFITI ZA SAYANSI ZINATHIBITISHA KWAMBA KIWANGO KIDOGO CHA ADHABU KWA MTOTO NI BORA ZAIDI NA HUMNUFAISHA ZAIDI.

WAZAZI NA WALEZI WANAPOKOSA UVUMILIVU HUSABABISHA WATOTO WAO KUFADHAIKA NA KUOGOPA BADALA YA KUPATA MAFUNZO KUTOKANA NA ADHABU WANAYOPEWA KWA AJILI YA MAKOSA WALIOTENDA.

TAAALUMA YA MISHIPA NA NEVA YA FAHAMU NA UBONGO INAONESHA KWAMBA UBONGO WA WATOTO HAUJAKOMAA KWA KIWANGO CHA KUTOSHA CHA KUWEZA KUHIMILI MSONGO WA MAWAZO. NI WAJIBU WA WAZAZI KUWA WENYE UVUMILIVU NA SUBIRA KWA WATOTO ILI KUWEZA KUWATULIZA.

KUKUZA UVUMILIVU NA UWEZO WA KUJITHIBITI KIHISIA HUSAIDIA UBONGO WA MTOTO KUKOMAA.

WATOTO AMBAO WAZAZI WAO WANAONESHA HASIRA NYINGI NI WAKALI, WENYE HUZUNI NA HUFANYA VIBAYA ZAIDI SHULENI KULIKO WENZAO KUTOKA FAMILIA ZENYE UTULIVU

KWA UPANDE MWINGINE, WATOTO AMBAO WAZAZI WAO HUWASHIRIKISHA ZAIDI BADALA YA KUWAADHIBU HUWA WENYE UELEWA NA USHIRIKIANO ZAIDI NA WAZAZI WAO.

UTAFITI UNATHIBITISHA KWAMBA WALE WATOTO WENYE SUBIRA HUFANYA VIZURI ZAIDI KULIKO WALE AMBAO HAWANA SUBIRA.



Kwa taarifa zaidi, tembelea:
www.unodc.org/listenfirst



Kwa hisani ya watu wa Ufaransa